

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA TATU**

**05 APRILI, 2018**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA TATU – TAREHE 05 APRILI, 2018

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

20. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE  
(MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara ya kutoka Mima hadi Mkanana ni mbaya sana na inapitika kwa shida sana wakati wote; na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa haina uwezo kifedha wa kuifanyia matengenezo makubwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara hiyo ili iweze kupitika wakati wote.

**21. MHESHIMIWA AGNES MATHEW MARWA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na tatizo kubwa la dawa katika Hospitali ya Manyamanyama iliyoko Wilayani Bunda na hii ni kutokana na Hospitali hiyo kutokuwa na hati rasmi ya kuwa Hospitali ya Wilaya:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaipa Hospitali ya Manyamanyama Hati rasmi ya kuwa Hospitali ya Wilaya ili kuongeza mgao wa dawa na kupunguza shida kubwa wanayoipata Wananchi;
- (b) Je, ni lini Serikali itaongeza Waganga na Wauguzi katika Hospitali hiyo ili kuongeza ufanisi.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**22. MHESHIMIWA KABWE RUYAGWA ZITTO  
(KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Mnamo tarehe 26/7/2017 Mawaziri wa Uchukuzi wa Uganda, Burundi, Congo DRC na Tanzania walifanya Mkutano katika Manispaa ya Ujiji Kigoma na kuazimia kuwa, kuanzia Januari

2018 Bandari ya Kigoma itakuwa Bandari ya mwisho kwa bidhaa za Burundi na Mashariki ya DRC (*Kigoma Port of Destination CIF Kigoma*). Pamoja na Azimio hilo, miradi ya Bandari ndogo za Ujiji na Kibirizi zilipaswa kujengwa na kuiwezesha miradi kama Ujiji *City- Great Lakes Trade and Logistics Center*:-

Je, Serikali mpaka sasa imefikia hatua gani ya kiforodha na kibandari kuiwezesha CIF Kigoma.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**23. MHESHIMIWA RUKIA KASSIM AHMED (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutokomeza vitendo vya udhalilishaji kwa Watoto.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI MKUU:**

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
05 APRILI, 2018**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**